

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Anwani ya simu: "MAKAMU",
Simu Na.: +(255)026 2329006
Nukushi.: +(255)026 2329007/2983150
Barua Pepe: km@vpo.go.tz



Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
S. L. P. 2502,
40406 DODOMA,
TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA

KANUSHO LA UKURASA BANDIA WA "GIVE DIRECT FOUNDATION" UNAODANGANYA WANANCHI KWA AHADI ZA UTOAJI FEDHA MTANDAONI KWA KUTUMIA JINA LA MAKAMU WA RAIS.

Kumekuwepo na taarifa za uwepo wa ukurasa wa Facebook unaojitambulisha kwa jina la Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Emmanuel Nchimbi, unaotangaza utoaji wa fedha kupitia Shirika la Give Direct Foundation. Ukurasa huo unaendelea kuwadanganya wananchi kwa kutumia picha ya Makamu wa Rais ili kuonekana kuwa rasmi na wa kuaminika.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotufikia, wananchi wanaelekezwa kuchagua kiwango cha fedha wanazohitaji na kulipia ada yake ya usajili ili kupata fedha hizo.

Kupitia taarifa hii, Ofisi ya Makamu wa Rais inautaarifu umma kuwa ukurasa huo hauna uhusiano wowote na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, hahusiki kwa namna yoyote na maudhui ya ukurasa huo wala matangazo yake.

Wananchi wanashauriwa:

1. Kutokujibu wala kufanya malipo yoyote kwa matangazo ya aina hiyo;
2. Kuripoti ukurasa huo moja kwa moja kupitia mfumo wa Facebook kwa kuchagua "Report Ad"; na
3. Kuwasiliana na Jeshi la Polisi au Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) endapo tayari wameathirika.

Imetolewa na
Ofisi ya Makamu wa Rais
15 Mei 2026.

